



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA WIZARA  
YA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA WAKALA  
WA USAJILI WA BIASHARA NA LESENI**



**Dar es Salaam - 13 JULAI, 2022**

**TAARIFA YA PILI KWA WAMILIKI WA MAKAMPUNI YALIYOSAJILIWA NCHINI**

***(Imetolewa chini ya Kifungu cha 400(2) cha Sheria ya Makampuni, Sura 212)***

Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) inaendelea na mchakato wa kuhuisha taarifa za Makampuni kwa njia ya Mtandao (Online Registration System). Zoezi hili linaenda sambamba na kusudio la Msajili wa Makampuni kuzifuta kampuni ambazo hazioneshi kuendelea kufanya biashara kwa kigezo cha kushindwa kuwasilisha Taarifa za mwaka (Annual Returns) kwa mujibu wa kifungu cha 128 cha Sheria ya Makampuni, Sura 212.

Tarehe 30 Mei, 2022, Msajili wa Makampuni alitoa Notisi ya siku 30 kwa kampuni zilizoorodheshwa kuthibitisha kama zinafanya biashara. Muda huo umekoma tarehe 30 Juni, 2022 ambapo Msajili wa Makampuni hakupokea taarifa ya kuthibitisha uwepo wa Kampuni kutoka kwa kampuni zilizoorodheshwa katika tovuti ya BRELA.

Msajili wa Makampuni anatoa Notisi ya pili kwa Kampuni zilizoorodheshwa hapa chini, kwamba endapo hatapokea uthibitisho wa kwamba kampuni hizo zinafanya biashara ndani ya siku thelathini (30) kuanzia tarehe ya kuchapishwa Notisi hii, ataendelea na hatua inayofuata ya kisheria ya kutangaza kwenye Gazeti la Serikali Notisi ya kuzifuta kwenye Daftari la Makampuni kwa mujibu wa kifungu cha 400(3) cha Sheria ya Makampuni, Sura 212.

Orodha ya Makampuni yanayokusudiwa kufutwa inapatikana kupitia [www.brela.go.tz](http://www.brela.go.tz).

**IMETOLEWA NA:**

**KITENGO CHA HABARI NA MAWASILIANO**